TAMKO LA BARAZA KUU TUGHE TAIFA
KWA VYOMBO VYA HABARI
KUHUSU KANUNI MPYA ZA MAFAO YA PENSHENI KWA WASTAAFU ZA MWAKA 2018

LEO TAREHE 21 DESEMBA 2018

JIJINI DODOMA

Utangulizi

Ndugu waandishi wa Habari,
Baraza Kuu Taifa la Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) tumekuwa na Vikao vyetu vya kikatiba hapa Jijini Dodoma kwa siku mbili (Tarehe 20 - 21 Desemba 2018) ambapo wajumbe wamepata fursa ya kujadili kwa pamoja masuala yanayohusu maslahi na ustawi wa Wanachama wetu na Watumishi wa Umma kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Katiba ya TUGHE ya Mwaka 1994 na Marekebisho yake Toleo la nne la mwaka 2015, sura ya pili ibara ya 2.0 (a) moja ya madhumuni makuu ya Chama chetu ni "**Kuboresha na kuendeleza hali nzuri ya Wanachama katika maisha yao wakiwa kazini na kuangalia maslahi yao wakishastaafu**".

Kwa kuzingatia dhumuni hili na mustakabali wa hatma ya maisha ya Wanachama wa TUGHE na Watumishi wa Umma kwa ujumla, Wajumbe wa Baraza Kuu tumelazimika kujadili kwa undani suala la Sheria ya PSSSF namba 2 ya mwaka 2018 pamoja na Kanuni mpya za Vikokotoo vya Mafao ya wanachama wastaafu wa Mifuko ya hifadhi ya Jamii zilizotangazwa na Waziri mwenye dhamana na kuanza kutumika kuanzia tarehe 01 Agosti, 2018.

Ndugu waandishi wa Habari,
Katika mjadala huo, Wajumbe wa Baraza kuu kwa kauli moja, tunapongeza kwa dhati kabisa na tunaunga mkono Kauli ya Kamati ya Utendaji ya TUCTA ya tarehe 5 Desemba, 2018

iliyotolewa Mjini Morogoro ambapo kwa pamoja Vyama vyote 13 vinavyounda Shirikisho (TUGHE tukiwa miongoni mwao) tulipinga vikali ujio wa kanuni mpya za Vikokotoo vya Mafao ya Wastaafu wa Mifuko ya hifadhi ya Jamii nchini na huo ndio msimamo wetu. Kimsingi Kanuni hizi zimepunguza kwa zaidi ya 62.5% ya malipo ya Mkupuo kwa mstaafu ikilinganishwa na Kanuni zilizotumika hapo awali za Vikokotoo vya **1/540** ***(Annual Accrual Factor)***, **15.5** ***(Commutation Factor)*** kadirio la miaka ya Uhai wa Mwanachama baada ya kustaafu, malipo ya nusu ya Pensheni ya Mwaka 50**%** ***(Commutation rate)*** kama malipo ya mkupuo na **50% inayobaki** kwa malipo ya pensheni ya kila mwezi.

Pamoja na kuunga mkono Tamko la Kamati ya Utendaji ya TUCTA, Baraza kuu la TUGHE Taifa tumetafakari na kuamua kwa pamoja kutoa kauli hii, kwanza kuonesha mshikamano wetu na Wafanyakazi na Wanachama wa Vyama vingine dhidi ya ujio wa Kanuni hizi ambazo tayari zimeonekana kutojali maslahi mapana ya Wafanyakazi wa Nchi hii hasa Watumishi wa Umma.

Ndugu waandishi wa habari

Chama cha TUGHE kama kinavyojieleza, ndicho chama kinachotetea maslahi ya Watumishi wa Umma katika Serikali kwa maana ya Wizara zote, Watumishi wa Bunge, Mahakama, Mamlaka za Serikali, Wakala wa Serikali na Watumishi wote wa Umma katika Serikali, Serikali za Mitaa na Taasisi binafsi wanaotoa huduma ya Afya kote Nchini. Kutokana na jukumu hili kuu la Chama chetu, Baraza Kuu ambalo ni Mamlaka ya juu ya Chama ya uamuzi ndani ya Chama imeona tusiishie katika kuunga Mkono Tamko la TUCTA pekee bali tueleze Watanzania pamoja na Serikali yetu juu ya nini hasa kinachowapata Wanachama na Watumishi wa Umma kutokana na ujio wa Kanuni hizi mpya za Vikokotoo.

HISTORIA FUPI YA HUDUMA ZA MIFUKO ILIYOKUWEPO

Ndugu Waandishi wa Habari

Ikumbukwe kwamba, awali Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iliundwa kulingana na Sekta za Wafanyakazi Nchini ambapo Mifuko iliyokuwa inatoa huduma za Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ilikuwa na Kanuni bora ikilinganishwa na Mifuko ya Hifadhi ya kada nyingine kutokana na sababu mbalimbali, mojawapo ikiwa ni tofauti ya viwango vya malipo ya Mishahara. Watumishi wa Taasisi na Mashirika ya Umma waliokuwa wakilipwa mishahara bora zaidi na walichangia katika mifuko ya PPF na GEPF na waliwekewa Kanuni zenye Mafao hafifu ikilinganishwa na PSPF na LAPF kwa sababu, mishahara na mazingira ya ustawi wao wakati wakiwa kazini ilikuwa ni bora kuliko ya Watumishi wa umma. Wafanyakazi katika Sekta binafsi walihudumiwa na wanaendelea kuhudumiwa na NSSF ambayo pia haikuwa na mafao bora ikilinganishwa na Mifuko ya PSPF na LAPF.

Watumishi wa umma katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa walioajiriwa kwa masharti ya Ajira za Kudumu na Malipo ya Uzeeni walianza kazi kwa malipo madogo sana ya mshahara ikilinganishwa na wale wa Mashirika ya Umma na Taasisi binafsi hivyo kuhudumiwa na Mifuko ya PSPF na LAPF ambayo iliwekewa kanuni bora za mafao kwa lengo la kufidia kile ambacho Watumishi hawa hawakuweza kukipata wakati wakiwa kazini kutokana na malipo madogo ya mishahara na mfumo wao wa kiutendaji kazi ambao haukuweka mazingira ya kuweza kujiandaa na maisha baada ya ajira.

Ndugu Waandishi wa Habari,
Baraza kuu la TUGHE tunaikumbusha Serikali pamoja na Jamii kwa ujumla kuwa, kuondolewa kwa Kanuni za zamani zilizokuwa na Mafao bora kwa mstaafu katika Sekta ya Umma na kuleta Kanuni mpya za kikokotoo limbikizi cha **1/580** ***(Annual Accrual Factor)***, Kadirio la miaka ya uhai wa Mwanachama baada ya kustaafu miaka **12.5** ***(Commutation Factor)***, malipo ya robo ya Pensheni kama mkupuo **25%** ***(Commutation rate)*** na **75%** kwa malipo ya pensheni ya kila mwezi zinazomnyang'anya Mstaafu malipo yake ya Mkupuo kwa zaidi ya 62.5% ni ukiukwaji wa dhana nzima ya kuanzishwa

kwa hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma PSPF (1999) na LAPF (2006) na uvunjwaji wa Mkataba wa ajira za Watumishi husika.

Baraza Kuu la TUGHE tumejadili na kubaini kuwa, kutokana na ujio wa Kanuni mpya za Vikokotoo vya Mafao, Wanachama wa iliyokuwa mifuko ya LAPF na PSPF wanaostaafu sasa watakumbwa na madhara yafuatayo:

1. Pensheni ya Mwaka itapungua kwa 6.9% ikilinganishwa na ile ya awali ya Kikokotoo cha **1/540** kutokana na matumizi ya Kikokotoo kipya cha **1/580.**

2. Malipo ya Pensheni ya Mkupuo (Kiinua Mgongo) yatapungua kwa 62.5% kutokana na kupunguzwa kwa kiwango cha malipo ya Mkupuo toka asilimia hamsini (**50%**) hadi asilimia ishirini na tano (**25%**) na kadirio la umri wa kuishi mstaafu toka miaka 15.5 hadi 12.5.

3. Mstaafu atakayefariki muda mfupi baada ya kustaafu atakuwa amelipwa robo ya mafao yake yaliyokadiriwa kwa miaka 12.5 pamoja na asilimia arobaini (40%) pekee kwa wafiwa kwa kipindi cha miaka mitatu. Hii itasababisha Wastaafu wengi kuacha kwenye mifuko kiasi kikubwa cha mafao ambayo walistahili na wangeweza kuyapata iwapo wangelipwa mkupuo mkubwa baada ya kustaafu.

4. Wanachama watapunguziwa mafao yao kwa viwango tofauti kulingana na kiasi cha mishahara katika kipindi cha miaka husika kutokana na Kanuni mpya kuondoa matumizi ya Mshahara wa Mwisho na badala yake kuleta matumizi ya wastani wa mishahara ya miaka mitatu kwa miaka kumi ya mwisho katika utumishi.

Ni wazi kuwa, kutokana na malipo duni ya mishahara kwa watumishi wa Umma, wengi wao hawakuweza kujenga makazi bora wakati wa Utumishi wao, matarajio yao yote yalikuwa kwenye malipo ya Mkupuo kwa kanuni bora za mifuko

waliyojiunga nayo wakati wa ajira ambazo sasa zimebadilishwa bila wao kupewa muda wa kujiandaa.

Ndugu Waandishi wa Habari,
Ili wanachama wetu waondokane na machungu yanayosababishwa na ujio wa Kanuni hizi, machungu ambayo yamesababisha manung'uniko na vilio vingi toka kwa Watumishi wa Umma na jamii nzima kwa ujumla ni vyema Serikali yetu sikivu inayoongozwa na **Mhe. Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** ikubali ushauri ufuatao:

i. Serikali ikubali pendekezo la kiungwana la kumaliza mgogoro huu wa Mafao kwa njia iliyopendekezwa na TUCTA ya kurejea katika meza ya Majadiliano.

ii. Pamoja na uwepo wa Mazungumzo hayo, Serikali itizame kwa mapana yake juu ya pendekezo la TUCTA la Mifuko kutumia Kanuni za 2017 *(The Social Security Schemes (Pension Benefit Harmonization) Rules za 2017)* ambazo zinatoa malipo ya Mkupuo wa **50%,** kikokotoo cha **1/540** na umri wa kuishi baada ya kustaafu miaka **15.5** kwa Wanachama wote waliokuwa katika Mifuko iliyoungana.

Hii itawasaidia Watumishi wa zamani ambao walianza kazi na mishahara midogo ikilinganishwa na sasa, kupokea malipo ya Mkupuo (Kiinua Mgongo) mazuri ikilinganishwa na Kanuni ya sasa hivyo kuwawezesha kujenga na kuboresha maisha yao ya uzeeni jambo ambalo walishindwa wakati wa Utumishi wao.

Ndugu Waandishi wa Habari,
Mifano ifuatayo inatoa picha halisi ya maelezo yetu katika tamko hili, na inaonesha kiasi cha mapunjo atakayopata Mtumishi wa Kima cha mshahara wa juu, kati na kima cha chini:

Hebu tuwaangalie watumishi waliostaafu baada ya kuchangia mfuko kwa miaka 30 wakiwa wamelipwa viwango tofauti vya mishahara:

Jedwali hili linalinganisha Mafao kwa Kanuni za Zamani na Mafao ya Kanuni za sasa.

Nd. Issa amestaafu akiwa na Mshahara wa Tsh. 1,000,000	**FAO**	**KABLA YA 2018**	**BAADA YA 2018**	**TOFAUTI**	**%**
	PENSHENI YA MWAKA	8,000,000	7,448,276	(551,724)	6.9
	KIINUA MGONGO	62,000,000	**23,275,862**	(38,724,138)	62.5
	PENSHENI YA MWEZI	333,333	465,517	132,184	-39.7
Nd. James amestaafu akiwa na mshahara wa Tsh. 300,000.00	**FAO**	**KABLA YA 2018**	**BAADA YA 2018**	**TOFAUTI**	**%**
	PENSHENI YA MWAKA	2,400,000.00	2,234,483	(165,517)	6.9
	KIINUA MGONGO	18,600.000.00	**6,982,759**	(11,617,241)	62.5
	PENSHENI YA MWEZI	100,000.00	139,655	39,655	-39.7
Nd. Masoud amestaafu akiwa na mshahara wa Tsh. 5,000,000	**FAO**	**KABLA YA 2018**	**BAADA YA 2018**	**TOFAUTI**	**%**
	PENSHENI YA MWAKA	40,000,000	37,241,379	(2,758,621)	6.9
	KIINUA MGONGO	310,000,000	**116,379,310**	(193,620,690)	62.5
	PENSHENI YA MWEZI	1,666,667.00	2,327,586	660,920	-39.7

Ukiangalia jedwali, ni dhahiri kuwa Watumishi hawa watalipwa mafao pungufu kwa 62.5% kama mkupuo ikilinganishwa na Kanuni ya Awali ya PSPF na LAPF. Pia asilimia ya kiwango cha madhara ya Kanuni hizi kwa Watumishi inalingana bila kujali ukubwa wa mshahara.

MAPUNGUFU KATIKA VYOMBO VYA UTATU VYA USHAURI

Ndugu Waandishi wa habari

Jambo jingine ambalo Wajumbe wa Baraza Kuu wamejadili kwa kina na kubaini mapungufu makubwa ni muundo na uendeshwaji wa Baraza la Utatu la Ushauri katika masuala ya Wafanyakazi nchini (LESCO). Baraza hili linaundwa na wawakilishi wanne (4) kutoka TUCTA, Waajiri (4), Serikali (4) na Wataalam wawili chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Muundo huu umeonesha mapungufu makubwa hasa linapojitokeza suala la mvutano kati ya Serikali na Wafanyakazi. Ni wazi kuwa uchache wa Wafanyakazi ndani

ya Baraza hili unasababisha Wafanyakazi wa Nchi yetu siku zote kupokonywa haki zao kutokana na uchache wao ndani ya chombo hiki kwa kupitishwa kwa maazimio yasiyojali uhalisia.

Zimekuwepo taarifa mbalimbali za upotoshaji kupitia vyombo vya Habari kuwa Wafanyakazi **walishirikishwa na walikubaliana** na mabadiliko ya Kanuni za Vikokotoo jambo ambalo si kweli. Wawakilishi wa Wafanyakazi walishirikishwa katika hatua zote muhimu lakini hawakukubaliana na Kikokotoo.

Ni vyema Wadau wakaeleza ukweli wa kile kilichotokea ndani ya LESCO badala ya kuudanganya Umma kuwa Wafanyakazi walishirikishwa na kukubali kutumika kwa Vikokotoo hivi. Wafanyakazi kupitia wawakilishi wa vyama vyao walishauri Serikali irejee katika Matumizi ya kanuni za 2017 ambazo SSRA walitangaza awali na ambazo hazikuleta taharuki kwa Wafanyakazi kutokana na kutowajumuisha wale wa zamani.

Ndugu waandishi wa Habari.
Kupitia tamko hili, TUGHE tunawaomba wanachama wetu na Watumishi wa Umma kote nchini kuwa **wapuuze madai ya kwamba Vyama vya Wafanyakazi tulikubaliana juu ya uwepo wa vikokotoo kandamizi**. Wawe na subira na kuendelea kufanya kazi zao kwa juhudi bila hofu yoyote kwani Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiongozwa na Mhe. **Rais Msikivu, mpenda ukweli na mwenye kujali maslahi ya Wanyonge Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli** itapokea mapendekezo ya Wafanyakazi.

Ndugu Waandishi wa Habari.
Tunapongeza kauli ya Waziri mwenye dhamana ya Kazi, Vijana Ajira, na Wenye Ulemavu **Mhe. Jenista Mhagama** (MB) ya kuwa tayari kukaa meza moja na Wawakilishi wa Wafanyakazi kwa lengo la kujadiliana kwa pamoja namna bora ya kuondoa sintofahamu hii kwa Wafanyakazi nchini lakini pia kuangalia namna bora ya uendeshwaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini kwa manufaa ya Wastaafu wa sasa na wale wa miaka ijayo.

TUGHE tunafahamu kuwa, mbali na madhara wanayopata Wanachama wetu kutokana na ujio wa Kanuni hizi, pia yapo madhara makubwa kwa upande wa Serikali na Jamii kwa ujumla ambayo si rahisi kuonekana kwa sasa, **madhara yanayotokana na kushuka kwa ari ya kujituma na ufanisi katika utendaji wa Watumishi wa umma kunakosababishwa na msononeko walio nao.**

Wafanyakazi wamebaki njia panda kutokana na ujio wa Kanuni hizi hasa kutokana na ukweli kuwa wengi hasa wale wa zamani hawakuwa wameandaliwa kukabiliana na hili. Kila mmoja amebaki akitafakari juu ya nini atafanya kuweza kukabiliana na Malipo hafifu ya Mafao ya Mkupuo badala ya kuelekeza akili na maarifa yao katika kuutumikia Umma. Ukubwa wa Madhara yatokanayo na hali hii hayawezi kuonekana kwa urahisi lakini malalamiko na manung'uniko ya Watumishi wa Umma kutoka pembe zote za nchi ni kiashirio tosha cha madhara haya.

Ndugu Waandishi wa Habari.
TUGHE tunamalizia kwa kusema kuwa, **tunaunga mkono kwa dhati kabisa juhudi zote zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano za kuhakikisha Nchi yetu inafikia malengo yake ya Uchumi wa Viwanda**. Tunampongeza Mhe. Rais pamoja na Serikali yake kwa Mafanikio makubwa ambayo tayari yanaonekana dhahiri.

Tanzania mpya tunayotarajia imeshaanza kuonekana ni vyema Sisi Watumishi na Wafanyakazi wa Nchi hii tuwe mstari wa mbele kushiriki na kuunga mkono juhudi za Serikali, wakati huo huo tukiangalia namna bora ya kupata Mafao yatakayotusaidia sisi na wategemezi wetu wakati tutakapostaafu.

Ahsanteni kwa kunisikiliza

Imetolewa na Baraza Kuu TUGHE Taifa na kusomwa mbele ya Waandishi wa Habari na **Nd. Archie Mntambo**, Mwenyekiti wa

Taifa wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE)

Saini ya Mwenyekiti wa TUGHE Taifa .....

"Huduma Bora, Maslahi zaidi"

(Ikumbukwe Tamko hili lilisomwa Tarehe 21 Desemba 2018 na siku 7 baadaye, tarehe 28 Desemba 2018, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt John Pombe Joseph Magufuli aliitisha Mkutano na Wawakilishi wa Wafanyakazi Ikulu Jijini Dar es Salaam na kutangaza kusitishwa kwa vikokotoo vipya na kutoa kipindi cha mpito cha miaka mitano (hadi mwaka 2023) wadau wawe wamepitia kanuni hizi na kuja na pendekezo la Kanuni itakayolinda Mifuko na wakati huo huo inamjali Mstaafu. Mchakato umeshaanza ambapo Kamati ya Wataalam inayoundwa na Wajumbe wa Utatu (Serikali, TUCTA na ATE) imeshaanza kazi ya kupitia upya Kanuni hizi kama ilivyoelekezwa na Mhe. Rais. Tuwe na matumaini kwani lengo la Serikali ni jema na hakika kanuni bora itakayolinda Mifuko na Mafao ya Wastaafu itapatikana).